

Hukumu- Umejiandaa?

Na William Emmanuel

Umejiandaa?

Tunaishi juu ya nchi katika siku ambazo watu wanaishi katika hatari ya kuchagua kusaka anasa za muda mfupi badala ya kuelekeza nia zao juu ya ulimwengu ujao. Hivyo, katika maisha haya watu hutafuta kuifikia ndoto yake binafsi, furaha bila kujali ukweli kuwa kesho wasasimama mbele ya kiti cha hukumu cha Mungu ili watoe hesabu ya maisha yao.

Hukumu ipo;

Biblia yaeleza waziwazi kuwa Mungu ameweka hali ya umilele ndani yetu, Mhubiri 3:11. Hata kama mtu anaweza kupiga teke na kukana uwepo wa milele, kukana hakuwezi kumwepusha mtu na jambo lijalo.

Jambo gani linalokuja? Kifo kinakuja! Na baada ya kifo kuja hufuatiwa na hukumu, Waebrania 9:27. Maana Mungu ameweka siku atakayouhukumu ulimwengu wote, Matendo 17:31. Yuda, nduguye na Yesu anaiita kuwa ni “hukumu ya siku ile kuu,” Yuda 1:6

Siku ni ya uhakika

Hakika unavyosoma makala hii leo ndivyo kwa hakika siku ya hukumu inasogea. Ukweli ni kuwa siku ya hukumu hairudishwi nyuma, haisemekani na haibadilishwi. Hakuna mamlaka yenye nguvu za kutosha kuisukumia mbali au kumfanya Mungu abadili nia yake. Haibadiliki hata mtume Paulo anairejea mara kwa mara akisema “siku ile,” “siku ile,” “siku ile,” katika 2Timotheo 1:12,18; 4:8. Yesu anaiita “siku ile,” “saa ile,” Yohana 5:28, na anasema saa inakuja ambayo wote waliomo makaburini watafufuka ili wakutane na kiti cha hukumu cha Mungu.

Siku hiyo ni kwa ajili ya kila mtu, ikimaanisha na wewe

Kila mtu tangu Adamu hadi mtu wa mwisho kuzaliwa duniani atasimama mbele za muumba siku hiyo. Yohana aliona “Wafu, wakubwa kwa wadogo, wamesimama mbele ya kiti cha enzi,” Ufunuo 20:12. Yaani, watu kutoka katika kila taifa maana “mataifa yote” ya dunia watakusanyika mbele zake, Mathayo 25:32. Na hiyo inakujumuisha na wewe, kwa kuwa “kila goti” litapigwa na “kila ulimi” utaapa, Isaya 45:23; Warumi 14:11; Wafilipi 2:10-11.

Uko tayari?

Leo tunasimama katika bonde la kukata maneno, Yoeli 3:14. Na kama Yoshua alivyowataka waisraeli kuchagua watakayemtumikia yapata miaka 3,500 iliyopita. Maisha yako ni maamuzi yako ya juu. Si tu kuchagua yupi wa kumuoa au wapi ukasome ama wapi ukaishi. Lakini, utamchagua Mungu au nafsi yako? Kama huna uhakika kumchagua Mungu ama nafsi yako ifanyaje na matokeo yake ni nini, leo kwa nini nafsi yako unaichezea kamali? Tafadhali, wasiliana nasi tukusaide kujibu swali hili leo!

